

HALMASHAURI YA WILAYA YA ULANGA. SHULE YA SEKONDARI IRAGUA.

YAH: MAAGIZO YA KUJUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IRAGUA WILAYA YA ULANGA
MKOA WA MOROGORO MWAKA 20.....

Jina la Mwanafunzi:.....

1.0:- Utangulizi.

Mkunu wa Shule, Shule ya Sekonari Iragua, anayo furahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujungana kidato cha KWANZA Mwaka 20..... katika **Shule ya Sekondari IRAGUA** iliyopo umbali wa takribani KM 80, kutoka makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ULANGA. Usafiri wa Mabasi kutoka mjini MAHENGE unapatikana katika kituo cha MABASI MAHENGE, Nauli ni Tsh 10,000/. Muhula wa kwanza masomo utaanza tarehe, Hivyo unatakiwa kuripoti shulenii kuanzia tarehe na mwisho wa kuripoti ni tarehe ndani ya siku saba.

2.0:- Mambo muhimu ya kuzingatia.

2.1:- Sare ya shule.

- a) Sare ya Shule hii ni Suruali na Sketi rangi ya DAMU YA MZEE, Shati rangi NYEUPE mikono mifupi
- b) **Kwa wavulana:-** TAI-(Punda Milia rangi ya Damu ya mzee na Nyeupe), SURUALI NA SHATI JEUPE Mikono Mifupi lenye Nembo, VIATU vyeusi vya kufunga na kamba, na Soksi nyeusi ndefu. **Maelezo ya mashono:-** SURUALI – Upana Chini uwe **INCHI KUMI NA SABA (17”)**.
- c) **kwa wasichana:-** TAI-(Punda Milia rangi ya Damu ya mzee na Nyeupe), SKETI NA SHATI JEUPE Mikono Mifupi lenye Nembo, VIATU vyeusi vya kufunga na kamba, na Soksi nyeupe ndefu au HIJABU(Rangi ya hijabu ifanane na sale ya shule ila HIJABU IFUNIKE PAJI LA USO, ISIWE YA KUBANA IWE NUSU KANZU IFIKE KWENYE GOTI NA SURUALI ISIWE YA KUBANA.)
Maelezo ya mashono:- SKETI – Mshono wa Rinda Boksi na iwe ndefu (**Iguse Viatu**).
- d) T-SHIRT ya Shule rangi Dark blue yenyewe Nembo ya Shule kwa wote

2.2:- Sare ya Michezo.

- a): Truck Suite/Suruali/Bukta na Fulana yake Rangi **NYEKUNDU** (b) Raba jozi moja rangi yoyote.

2.3:- Sare za kazi.

- a): Sketi/Suruali rangi Nyeusi. (b): T-Shirt yenye Nembo ya Shule rangi ya Udongo.

2.4:- Vifaa vya Darasani.

:(i):Madaftari Makubwa Kumi na mbili (12) ya Counter Book. (ii):Mkebe mpya (Mathematical Set). (iii):Kamusi ya Kiingereza(Dictionary).(iv):Begi la kubebia Daftari.

3.0:- Sheria za Shule:

A: HESHIMA

- i. Mwanafunzi anatakiwa kusimama na kumsalimia mwalimu au mtu yeyote anaye mzidi umri
- ii. apitapo,anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano
- iii. Mwanafunzi haruusiwi kutumia Lugha mbaya wakati wowote kati yao wenyewe, kwawalimu wao au kwa watu wengine.
- iv. Mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu wafanyakazi wote waliopo shulenii
- v. Mwanafunzianapaswakushirikiananakusaidiakatikakazi
- vi. Mwanafunzi anapaswa kuthamini kazi za ainazote shulenii
- vii. Mwanafunzi haruhusiwi kufanya mambo yafuatayo:
 - a) Kuvuta Sigara
 - b) Kufuga Kucha, Ndevu na Nywele
 - c) Kuvaavazi yasiyo ya heshima
 - d) Kugombana
- viii. Mwanafunz ianatakiwa kuitika mara moja na kukimbilia aliko mkuu aliyemuita
- ix. Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu Bendera ya Taifa, Picha za viongozi wa Serikali, Nembo ya Taifa. Wimbo wa Taifa na Fedha za Taifa
- x. Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu Ofisi za Shule, Mali binafsi na Mali ya umma.
- xi. Mwanafunzi anatakiwa kusimama katika mstari wakati wa kupokea huduma
- xii. Mwanafunzi anatakiwa kukaa kimya wakati wote akiwa darasani, asitoke nje bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyeko.

B: MAHUDHURIO

- i. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria shule kwa muda wote wa masomo
- ii. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa
- iii. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria katika kazi zote za mikono
- iv. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria mikutano ya shule kama Baraza la shule, ukaguzi wa Usafi, kupandisha bendera ya Taifa.

C:MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.


- i. Wizi wa aina yoyote.
- ii. Uasherati, ubakaji na ushoga.
- iii. Ulevi na matumizi ya Madawa ya kulevya.
- iv. Uvutaji bangi.

- v. Utoro wa siku 90 mfululizo.
- vi. Kutokufanya Mitihani na Majaribio.
- vii. Kukutwa na Simu na Matumizi ya Simu katika Mazingira ya shule.
- viii. Kupigana au Kupiga
- ix. Kuharibu kwa makusudi Mali ya Umma.
- x. Kudharau Bendera ya Taifa
- xi. Kutembelea Sehemu za Starehe kama Bar, Guest na Vibanda vya Video.
- xii. Kuoa au Kuolewa.
- xiii. Kupata Mimba au kusababisha Mimba ndani na nje ya shule.
- xiv. Kutoa Mimba
- xv. Kugoma, Kuchochea na Kuongoza au Kuvuruga amani na Usalama wa Watu.
- xvi. Kukataa Adhabu kwa makusudi.

Hivyo anatakiwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za shule ili aweze kuendelea kuwa Mwanafunzi wa Iragua Sekondari.

TANIBIHI:- Hakikisha umepima Afya yako na Fomu hiyo (Medical Examination) unapaswa kuirudisha Shuleni pindi unapo mleta mtoto .

NAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA
KARIBU SANA IRAGUA SEKONDARI.


.....
ELIAS K. SAMWEL.

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI IRAGUA
S.L.P. 264
IFAKARA

MKUU WA SHULE.